# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
# OFISI YA RAISI-TAMISEMI
# SHULE YA SEKONDARI IHANU S.L.P 337-MAFINGA

**JINA LA MWANAFUNZI** _____

## YAH; MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IHANU WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

## 1.0 UTANGULIZI.

- Napenda kutumia nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuingia **KIDATO** cha **KWANZA** katika shule hii ya **IHANU** Sekondari.
- Shule hii ipo katika kijiji cha **Ibwanzi** katika kata ya **Ihanu**, Tarafa ya **Ifwagi**, Wilaya ya **Mufindi**, Mkoa wa **Iringa**.
- Hali ya hewa ni ya baridi kiasi na ni nzuri kwa masomo.

## 2.0 KUFUNGUA SHULE

- Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**, Kila mwanafunzi atatakiwa kufika shuleni siku hiyo bila kukosa akiwa na mahitaji yote ya shule kama alivyo agizwa.
- Shule ya sekondari Ihanu ni ya kutwa na ni mchanganyiko wa wavulana na wasichana.

## 3.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA.

Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni Hisabati, Jiografia, Uraia, Historia, Baiolojia, Kiswahili, Kiingereza, Fizikia, Kemia pamoja na somo la dini ambalo kila mwanafunzi atahudhuria vipindi vya dini yake.

## 4.0 VIFAA VYA TAALUMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:-

- Madaftari 10.
- Mkebe wa Hisabati (Matrhematics).
- Kalamu za wino (pen) bluu na nyeusi.
- Penseli na mfuto.
- Rula.

## 5.0 SARE YA SHULE

### 5.1 SARE YA WAVULANA.

1. Suruali mbili (2) nyeusi zilizoshonwa vizuri.
2. Shati nyeupe (teroni) mbili (2) ziwe na mikono mirefu.

3. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi (***BOOTS HAZIRUHUSIWI KABISA)*** vyenye kamba.
4. Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe au brown.
5. Sweta mbili (2) rangi ya kijani (jani la mgomba).
6. Tai mbili (2) rangi nyeusi.
7. Raba ya michezo jozi moja (1).
8. Trakisuti rangi nyeusi ufito mweupe mbili (2) (zitavaliwa muda wa michezo na kazi za nje).
9. T.shirt mbili (2) rangi blue.

## 5.2 SARE YA WASICHANA

1. Sketi mbili (2) za rangi nyeusi zenye marinda ya kawaida zishonwe kwa heshima na ziwe ndefu kupita magoti.
2. Shati nyeupe (tetroni) mbili (2) ziwe na mikono mirefu zisizo onyesha mwili (transparent).
3. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi (***BOOTS NA VIATU VYENYE KISIGINO HAVIRUHUSIWI KABISA)*** vyenye kamba.
4. Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi.
5. Sweta mbili (2) rangi ya kijani (jani la mgomba).
6. Tai mbili (2) rangi nyeusi.
7. Raba ya michezo jozi moja (1).
8. Trakisuti rangi nyeusi ufito mweupe mbili (2) (zitavaliwa muda wa michezo na kazi za nje).
9. T.shirt mbili (2) rangi ya blue.

# 6.0 VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA SHULENI.

- Ndoo moja mpya ya ujazo wa lita kumi.
- Jembe moja jipya lenye mpini (kwaajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe akiwa shuleni.
- Rimu ya karatasi **A4**.

NB: maagizo mengine yataamuliwa na vikao vya wazazi/ walezi kama michango ya chakula n.k

# 7.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miiongozo yote inayotolewa na **Wizara ya Elimu Sayansi na tecknolojia** yenye dhamana ya Elimu nchini na **Ofisi ya Rais-TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafa1nuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumlas ni jambo la lazima.

Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

A. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
B. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

C. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa wanafunzi wako katika shule hii.
D. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira yote ya shule.
E. Kuvaa sare ya shule wakati wote inapotakiwa.
F. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
G. Kutunza mali za umma.

## 8.0 MAELEZO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA.

A. Inasisitizwa kwamba kila mwanafunzi aje na mahitaji yote la sivyo hatapokelewa.
B. Kila mwnafunzi analazimika kutii kuheshimu sheria zote na taratibu zake.
C. Kila mwanafunzi inamlazimu awapo shule kujifunza na kujua wimbo wa shule, wimbo wa Taifa na wimbo wa Tanzania nakupenda.
D. Kila mzazi/mlezi na mwanafunzi husika inamlazimu kujaza (KIAMBATANISHO A) kwa ukamilifu na kuleta mara shule inapofungua.
E. Cheti cha kuzaliwa (kivuli chake).
F. Cheti cha afya toka kwa daktari (KIAMBATANISHO B).

## 9.0MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- Kujichubua na kutumia vipodozi ni kosa linaloweza kusimamisha shule/ kufukuzwa shule.
- Kukata sketi ili iwe fupi au kuvaa sketi fupi, kuvaa suruali zinazoonyesha makalio (mlegezo) au suruali zinazobana (model) unaweza kupewa adhabu za ndani au kusimaishwa masomo.
- Wizi.
- Uasherati na ushoga.
- Ubakaji.
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, sigara, kubeli na kadhalika.
- Kupigana ama kupiga.
- Kuharibu makusudi mali za umma.
- Kudharau bendera ya taifa.
- Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba kwa wavulana.
- Kuoa ama kuolewa.
- Kutoa mimba.
- Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvurugu amani na usalkama wa shule au watu.
- Kukataa adhabu kwa makuzudi.
- Kuwa na simu ya mkononi (kumiliki na kutumia ukiwa shuleni).

NB:- Sheria na taratibu nyingine zote mwanafunzi atasomewa akifika shuleni

## "KARIBU SANA IHANU SEKONDARI KWANI ELIMU NI UKOMBOZI"

**……..**
***ESPEDITO NDALE***
**MAKAMU MKUU WA SHULE**

KIAMBATANISHO ‘A’

Jina la kijiji _____

Anuani S.L.P _____

TAREHE: _____

**MKUU WA SHULE,**
**SHULE YA SEKONDARI IHANU,**
**S.L.P 337,**
**MAFINGA.**

## YAH; KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHANU.

1. Mimi (jina la ***mzazi/mlezi***) _____.
2. Nakubali mwanangu ajiunge na shule hii na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake kama ilivyoagizwa kwenye maelekezo ya kujiunga na shule.
3. Naahidi kumuhudumia motto wangu kwa hali na mali ili kufanikisha malengo yake ya kujiunga na shule hii ya Ihanu sekondari.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake ya taaluma muda wote awapo shuleni

**SAHIHI: _____ TAREHE: _____**
**NAMBA YA SIMU:_____**

Mimi _____
kujiunga na shule hii kidato cha kwanza mwaka **2021.** Naahidi kuwa mtiifu na kufuata sheria za shule na kuwa na nidhamu ya kujituma kusoma kwa bidii kuwa mfano bora kwa wanafunzi wenzangu ili nifike malengo ya shule hii. Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

**SAHIHI: _____ TAREHE:_____**

KIAMBATANISHO ‘B’

**SHULE YA SEKONDARI IHANU,**
**S.L.P 337,**
**MAFINGA.**

**DAKTARI _____**
**HOSPITALI YA _____**
**S.L.P _____**
**_____**

## YAH; FOMU YA KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI

Tafadhari tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi/mlezi wake na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya Sekondari katika shile hii.
Ni muhimu kabla ya kuja hapa ili kujua afya yake.

_____

***ESPEDITO NDALE***
**MAKAMU MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI IHANU**.

**MKUU WA SHULE,**
**IHANU SEKONDARI,**
**MAFINGA.**

**YAH; MWANAFUNZI** _____

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi alietajwa hapo juu.

1. Urine _____
2. Stool _____
3. HB _____
4. Pregnancy test _____
5. Spleen _____
6. Chest _____
7. Eyes _____
8. Ears _____
9. Physical abnormality

   _____

   _____
10. _____

    _____

    _____

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu

_____

_____

Ataweza/ hataweza kumudu masomo ya sekondari

| _____ | _____ | _____ | _____ |
|---|---|---|---|
| **JINA LA DAKTARI** | **CHEO** | **SAHIHI** | **TAREHE** |